

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
WAKALA WA MAJENGO TANZANIA
Sokoine Na.2 Mkabala na Ukumbi wa Karimjee

Anuani ya Simu "MAJENGO" Dar es
Salaam.
Namba ya Simu: **022-2117114/2122163**
Nukushi: **022-2114143/2122370**
Barua pepe: **ce@tba.go.tz**
Tovuti: **www.tba.go.tz**



S.L.P. 9542,
Dar es Salaam.

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

MAELEZO KUHUSU NYUFA ZILIZOTOKEA KWENYE JENGO LA BLOCK "A" KATIKA HOSTELI MPYA ZA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

1.0 UTANGULIZI

Tarehe 03 Disemba, 2017 kuliripotiwa kutokea kwa Nyufa kadhaa kwenye Hosteli mpya za Chuo Kikuu cha Dar es salaam, zilizobuniwa na kujengwa na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Taarifa hizo zilisambaa kupitia Mitandao mbalimbali ya Kijamii kiasi cha kuleta hofu na wasiwasi kwa watumiaji wa Majengo hayo na jamii kwa ujumla.

Lengo la Taarifa hii ni kueleza sababu za kutokea kwa Nyufa hizo na hatua ambazo TBA imezichukua.

2.0 MAELEZO KUHUSU SABABU ZA KUTOKEA KWA NYUFA

Baada ya kupata taarifa hizi, wataalamu wa TBA walifanya ukaguzi kwenye Majengo hayo Tarehe 03 Disemba, 2017 na kubaini kuwa Nyufa zimetokea kwenye (Expansion joint) iliyopo Block A. Kwa kawaida katika taaluma ya ubunifu wa Majengo, Majengo mapana huwekewa nafasi (Expansion joint) ambayo huyatenganisha na kuwa sehemu mbili au zaidi ili kuruhusu Jengo kupumua inapotokea kutitia kwa udongo, au kutanuka na kusinyaa kwa udongo kutokana na hali ya hewa. Kwa maneno mengine, (Expansion joint) ni sehemu ambayo inatarajiwa Nyufa kutokea.

Katika ubunifu wa Majengo haya, TBA ilizingatia hitaji hilo ambapo kila jengo (Block) lina jumla ya (Expansion joint) tatu (3). Katika jengo la Block A, nyufa zilizotokea ziko kwenye (Expansion joint), kwa hiyo, siyo kwa

sababu ya upungufu wa ubunifu au ujenzi bali umetokea katika maeneo yaliyokusudiwa (Expansion joint).

3.0 HATUA AMBAZO TBA IMEZICHUKUA

Katika ukaguzi wa awali uliofanywa na wataalamu wa TBA, ilionekana upande mmoja wa ile (Expansion joint), uko vizuri kwani ule uwazi (Gap) umeonekana kufunikwa na kipande cha ubao bila kujazwa na udongo wa Saruji. Ila upande wa pili wa ule uwazi ulijazwa kimakosa na udongo wa saruji na kuondoa urahisi wa sehemu mbili za jengo kupumua. Upande wa pili wa uwazi uliojazwa udongo ndiyo unaoonyesha dosari ya Nyufa zilizojitokeza, kutokana na ripu kwenye ukuta mzima wa sehemu ile kuungana na ule udongo ulioingia kwenye (Expansion joint).

Kwa taaluma ya ujenzi wa majengo, dosari hii ni ya kawaida kutokea, kwahiyo Wakala wa Majengo (TBA), umeanza kuchukua hatua za haraka kusahihisha kwa kuhakikisha kuwa ule uwazi (Expansion joint) unakuwa huru bila kujazwa na kitu kigumu. Sehemu za ukuta zinazopakana na hiyo (Expansion joint), nyufa zake zitarekebishwa. Na kwa Majengo mengine yatahakikiwa kuhakikisha kuwa (Expansion joint) ziko huru bila kuingiwa na kitu kigumu.

4.0 MWISHO

Kwa maelezo hayo hapo juu TBA inapenda kuwatoa hofu watumiaji wote wa majengo hayo kuwa ni salama kwa matumizi yaliyokusudiwa na kwamba; nyufa zilizotokea ni za kawaida katika ujenzi wa Majengo na zimetokea sehemu iliyokusudiwa ambayo itafanyiwa marekebisho stahili.

**IMETOLEWA NA MTENDAJI MKUU
WAKALA WA MAJENGO TANZANIA (TBA)
04 DISEMBA, 2017**